# CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI NA ELIMU YA JUU SAYANSI, TEKNOLOJIA, UFUNDI STADI, HABARI NA UTAFITI (RAAWU)

RESEARCHERS, ACADEMICIANS & ALLIED WORKERS UNION

RAAWU

# KIJUE CHAMA CHA WAFANYAKAZI CHA RAAWU

## 1. MAANA YA CHAMA CHA WAFANYAKAZI

Ni muungano wa Wafanyakazi wa sehemu au sekta husika ya kazi, unaotokana na ridhaa yao wenyewe kwa lengo la kulinda, kutetea haki na maslahi yao. Muungano huu hatimaye hutambuliwa rasmi na mamlaka ya nchi baada ya kusajiriwa kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo. Kwa Tanzania Sheria namba 6 na 7 za mwaka 2004 ndizo zinayosimamia vyama vya wafanyakazi.

## 2. MAANA YA RAAWU

RAAWU ni kifupisho cha maneno ya Kiingereza "Researchers Academicians and Allied Workers Union". Neno hili limetafsiriwa Kiswahili kukidhi matakwa ya wanachama wetu; yaani Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi ya Elimu ya Juu, Sayansi, Teknolojia, Ufundi Stadi, Ushauri, Habari na Utafiti.

## 3. KUUNDWA KWA RAAWU

Kuundwa kwa RAAWU kulitokana na mabadiliko katika historia ya Vyama vya Wafanyakazi nchini, kutoka katika mfumo wa chama kimoja cha wafanyakazi NUTA/JUWATA (1964-1991) na kuingia kwa mfumo unaoruhusu Wafanyakazi kujiundia Vyama vyao kulingana na sehemu au sekta wanazotoka.

RAAWU ni miongoni mwa vyama huru kumi na moja (11) viliundwa chini ya Sheria ya OTTU namba 20 ya mwaka 1991. Mkutano Mkuu wa kwanza wa RAAWU uliofanyika mwezi Novemba 1994, ndio uliohitimisha uundaji wa chama hicho baada ya kupitisha katiba na kuchagua viongozi wa kitaifa.

RAAWU vilevile ni Chama huru kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Wafanyakazi No. 10, 1998. Mwaka 2000 RAAWU iliitisha Mkutano Mkuu wa Tatu ambao ulifanya marekebisho ya Katiba na Kuchagua viongozi wapya wa kitaifa. Aidha mkutano huo ulipitisha maazimio kadhaa yanayolenga katika kuboresha maisha ya Wanachama na jamii kwa ujumla.

## 4. DIRA YA RAAWU (VISION)

Kuwepo kwa jamii ambamo watu wana haki ya kufanya kazi, Vyama imara vya Wafanyakazi vinavyoendeshwa kidemokrasia na kuhakikisha wafanyakazi wanapatiwa mahitaji yao ya kijamii na kiuchumi.

## 5. LENGO LA RAAWU (MISSION)

Lengo la RAAWU ni kuboresha mazingira ya kazi kwa wanachama wake, kushirikisha wanachama katika kufikiwa kwa maamuzi ya chama, kushinikiza juu ya kuwepo kwa sera zitakazoinua na kukuza nafasi za ajira na kuhakikisha kwamba wafanyakazi wanakuwa na maisha bora wakiwa kazini na baada ya kustaafu.

## 6. RAAWU imejishirikisha na:-

(a) Shirikisho la Syama vya Tafanyakazi Tanzania (TUCTA).

(b) Shirikisho la kimataifa linalohudumia wafanyakazi wa Sekta za Huduma kwa Umma "Public Services Interational" (PSI).

## 7. MADHUMUNI YA RAAWU

(a) Kuboresha na kuendeleza hali nzuri ya wanachama katika maisha yao wakiwa kazini na baada ya kustaafu.

(b) Kushirikiana na kujadiliana na waajiri katika kudumisha amani mahala pa kazi.

(c) Kujadiliana na kuondoa tofauti zinazojitokeza baina ya mwajiri na mwanachama, au mwanachama mmoja na mwingine kwa njia ya makubaliano ya amani kadri inavyowezekana.

(d) Kushiriki katika kusaidia utekelezaji wa mikataba ya hali bora za kazi, tuzo, kanuni za nidhamu na kanuni zozote zile ambazo zinatumika nchini.

(e) Kushirikiana na kubadilishana ujuzi na vyama vingine vya wafanyakazi nchini pamoja na vile vya Kimataifa.

(f) Kuwasiliana na Serikali kuhusu utungaji wa sheria sahihi za kazi na kuandaa sera nzuriza kuendeleza maisha ya jamii.
(g) Kulinda maslahi ya wanachama kwa kuhimiza Serikali kuepukana na uandaaji wa sera ambazo ni hatari kwao.

## 8. UANACHAMA

RAAWU inahamasisha wafanyakazi katika taasisi zifuatazo:-

(a) Taasisi za Elimu ya Juu
(b) Taasisi za Utafiti.
(c) Taasisi za Ufundi Stadi (VETA).
(d) Taasisi zinazojihusisha na masuala ya Sayansi na Teknolojia.
(e) Taasisi za ushauri (Consultancy).
(f) Taasisi za Habari na
(g) Taasisi za Kimataifa.

Wafanyakazi katika sekta zote zilizotajwa hapo juu wanayo haki ya kujiunga na kuwa wanachama wa RAAWU.

Hadi kufikia mwezi Desemba 2008 RAAWU ina wanachama wapatao 11,988 na wanachama watarajiwa wanakadiriwa kuwa 8,000.

## 9. NAMNA YA KUJIUNGA NA RAAWU

Kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Namba 6 na 7 ya mwaka 2004 wafanyakazi wapatao kumi mahala pa kazi wanayo haki ya kuunda tawi la chama chao husika.

Taarifa za kutaka kuunda tawi zitawakilishwa kwa Katibu wa Kanda/ Mkoa husika ambaye atasaidia kufanikisha uundaji huo kwa mujibu wa katiba ya chama.

Mwanachama mpya anayejiunga na RAAWU atakabidhiwa kadi yake ya uanachama, ambayo kwa sasa inatolewa bure. Mahali ambapo tayari pana tawi, Mwanachama anayetaka kujiunga atakwenda ofisi ya RAAWU ya Tawi ambapo ataandikishwa kwenye

kitabu cha orodha ya wanachama na kukabidhiwa kadi ya chama.

## 10. WAJIBU WA MWANACHAMA

(a) Kulipa ada ya kila mwezi kwa kiwango kitakachokuwa kimeamuliwa na wanachamawenyewe kupitia wawakilishi wao.
(b) Kuunga mkono na kusaidia kwa vitendo maendeleo ya chama.
(c) Kuzingatia kanuni na taratibu za chama na kuheshimu maamuzi yanayotokana na anuni au taratibu hizo.

## 11. MANUFAA YA KUJIUNGA NA RAAWU

Mfanyakazi atakayejiunga RAAWU:-

(a) Haki zake za ajira zitalindwa na Chama
(b) Atakuwa na haki ya kutetewa na Chama katika chombo chochote kile kinachotoa haki pale itakapodhihirika kuwa ameonewa na mwajiriau kiongozi wake wa kazi kwa gharama za chama.
(c) Maisha yake kazini yataboreshwa kupitia mikataba ya hali bora za kazi inayotokana na majadiliano ya pamoja baina ya Chama cha Wafanyakazi na Waajiri au serikali. Mikataba hii humwezesha mwanachama kupata maslahi bora zaidi mbali na yale yaliyowekwa kisheria.
(d) Atakuwa na kauli zaidi mahali pake pa kazi kwani kwa kupitia Chama, maoni au ushauri wake utasikika.
(e) Atapata elimu na maarifa mbalimbali yatolewayo na chama yenye manufaa kwa maisha na ajira yake.
(f) Atapata fursa ya kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika Chama na kuwakilisha wenzake kwenye vyombo mbalimbali vinavyohusika na masuala ya wafanyakazi.
(g) Atashiriki katika shughuli zote za Chama kwa mujibu wa Katiba na Kanuni za Chama.
(h) Hali yake ya maisha itaboreshwa kupitia miradi mbalimbali ya kiuchumi inayoanzishwa na

na Chama sehemu za kazi kwa lengo la kuwapunguzia wafanyakazi makali ya maisha.

(i) Masuala yanayohusiana na nyongeza za mishahara, marupurupu, kuthibitishwa kazini, kupanda madaraja, mifuko ya hifadhi ya jamii na mafao mbalimbali yatafuatiliwa na kufanikishwa na Chama.

(j) Atahakikishiwa mazingira bora ya kazi yanayozingatia kanuni za afya na usalama mahali pa kazi.

(k) Mfanyakazi mwanamke atapata fursa ya kuungana na wanawake wenzake nadani ya Chama na hivyo kushiriki katika kuendeleza harakati za ukombozi wa wanawake nchini na duniani kote.

## 12. MAFANIKIO YA RAAWU

(a) RAAWU imefanikiwa kuongeza matawi mapya kutoka matawi 156 mwaka 1995 hadi matawi 261 Desemba 2013.

(b) Idadi ya wanachama nayo imeongezeka kutoka wanachama 4693 mwaka 1995 hadi wanachama 12,480 mwaka 2013.

(c) RAAWU iliwasilisha mahakamani pendekezo la kufutwa kwa Kodi ya Maendeleo kutokana na mfumo wa kodi hiyo kutokuwa na haki kwa wafanyakazi. Hatimaye serikali ilifuta kodi hiyo.

(d) RAAWU imeshiriki katika kushinikiza marekebisho ya mifuko ya hifadhi ya jamii hasa PPF na NSSF. Mifuko hiyo imefanyiwa marekebisho ya kutungiwa Sheria ingawaje bado ina kasoro ambazo RAAWU inaendelea kuzifuatilia.

(e) RAAWU imetoa mchango mkubwa kwenye marekebisho na utungaji wa sheria mbalimbali za kazi.

(f) RAAWU imeshiriki kuandaa sera ya Vyama vya Wafanyakazi kuhusu UKIMWI.

(g) RAAWU imeshiriki katika kushinikiza ushirikishwaji kwenye uandaaji na utekelezaji wa sera za kuondoa Umaskini nchini na Ushirikishwaji katika suala zima la ubinafsishaji.

(h) RAAWU imenunua eneo lenye ukubwa wa mita za mraba huko TUANGOMA Dar es Salaam kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi ili kusaidia ajira kwa vijana.

(i) RAAWU imeshatoa elimu ya sheria mpya za kazi katika mikoa yote ambayo kuna matawi ya RAAWU.

(j) RAAWU imeshiriki kikamilifu katika mchakato wa kupigania kupandishwa vyeo na kuthibitishwa kwa watumishi wa serikali.

(k) RAAWU imepigania nyongeza ya mishahara ya watumishi wa umma.

(l) RAAWU imekamilisha uanzishwaji wa ofisi za Kanda zote. Ofisi hizo zina vitendea kazi vya kutosha yakiwemo magari na kompyuta kwa kila Kanda.

## 13. MIPANGO YA BAADAE YA RAAWU

(a) Kuhakikisha kuwa Sheria Mpya za Kazi namba 6 na 7 zinafahamika kwa viongozi na wanachama katika matawi yote.

(b) RAAWU kuwa na jengo lake la ofisi na ukumbi wa mikutano.

(c) Kushirikiana na TUCTA na Vyama vingine vya Kimataifa, katika kupigania maslahi na mazingira bora ya kazi.

(d) Kuwashawishi wanachama wanawake kujitokeza na kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika Chama.

(e) Kuboresha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na kuendeleza hali nzuri ya wanachama katika maisha yao wakiwa kazini na baada ya kustaafu.

(f) Kushirikiana na kujadiliana na waajiri katika kudumisha amani mahala pa kazi.

(g) Kuhamasisha wafanyakazi wote walio kwenye sekta za RAAWU kujiunga na Chama.

(h) Kutoa taarifa za mara kwa mara kuhusu Chama kwa wanachama na wasio wanachama

(I) Kujadiliana na kuondoa tofauti zinazojitokeza baina ya mwajiri na mwanachama, au mwanachama mmoja na mwingine kwa njia ya makubaliano ya amani kadri inavyowezekana.

(j) Kushiriki katika kusaidia utekelezaji wa mikataba ya hali bora za kazi, tuzo, kanuni za nidhamu na kanuni zozote zile ambazo zinatumika nchini.

**RAAWU Headquarters**
**Bibi Titi/Sophia Kawawa Street**
**P. O. Box 22532**
**Dar-es-Salaam**
**Tel: +255 22 2123762**
**Fax: +255 22 2123762**
**Mobile +255 767 123762**
**+255 786 123762**
**+255 716 123762**
**Email: raawutanzania@gmail.com**
**Website: www.raawu.or.tz**